**Agnes Kisoo:** Kwou mathina ala twinamo nikukulya ii tene twitawaa niki? Tutlistini ya syindu na nengi twenuka nitusuania mo nimenuka malika ngalini naitu tuyinuka na maau tuyithia syana ikomie na mbui kithekani na utethyo tuiwona wa kwinuka kana wa kuthi

**Translator :** Wanauliza ni kwa nini wanaitwa kuimba kama hawapatiwi chochote na warudi nyumbani wanafika usiku wanapata watoto wamelala hakuna chakula na wanafikiria wale wamewaita wameenda salama.

**Agnes Kisoo :** we mundu usu utwitaa no utumathia utethyo ni kana tukona tikakuwa ni ngali kana akatumathia utethyo tukasyomethya syan isu?

**Translator :** Wanauliza kwanini huyo anawaita hawatafutii njia za kusomesha watoto ama za kutafuta gari.

**Agnes Kisoo:** niki kusomethya syana na vandu va kumathiwa wia isyoka nyumba tuyuka kuima nayu syana syitu ni kuima natiu nitukuima mathina maingi tuina mano twaiwaa nula unutuluthya nundu syana syi o musyi

**Translator :** Pia anauliza ni kwanini wanasomesha watoto na wakimaliza shule hawapati kazi wanarudi nyumbani kulima na wao.

**Agnes Kisoo:** nitakwasya ethiwa nimutonya andu ma Katiba nikutwosele vau nengi ko ve undu ute pension, tene mundu athukuma akua tyo ununengwa retire na inewa pension aithi utethya andu ma musyi

**Translator :** Wanasema kama inawezekana waangaliwe sababu sasa wamekuwa wamama na wanataka pension.

**Agnes Kisoo:** mo andu asu matwitaa tumainia no matataa kwona mathina ma kutwita twi akuu tukaenda nthi yiana uu na tuisyoka tuikomboa ngali tuyuka musyi, ithye ene tukunite ndii

**Translator :** Wanauliza kwanini hawa wanawaita kuwambia hawaoni shida yao na wao ni mama wawatafutie kama ni gari au ama wapatiwe usaidizi.

**Agnes Kisoo:** na nundu katiba na ndeto ila ingi syonthe nota iia tuandike, mweitwosele ethiwa vai maana ma kuvituka vau nisyiwa twiwe twikale nthi tuthiane o vau musyi

**Translator :** Wanasema muwachukulie at their level na waachwe wapumzike nyumbani

**Agnes Kisoo :** nundu andu asu namainia na neetwa namatwaia valua twathi nimungulya liu nakwa ndina mbesa na ndinaetewa na twika umenania vau, tumathiwe nzia ila tutonya uthi nayo

**Translator :** Sababu kama Chairlady akipata barua ya invitation, anapeleka kikundi chake na hawapati chochote, na wakirudi nyumbani sasa complaint inanza kukuja kwake. Kwanini amewapeleka na hakuna chochote?

**Agnes Kisoo :** kwou kikundi kii naambiie ni maeo nayu ndi maeo na ninikue e na noniendee naitwa na ndina utethyo ii yu kondmosetwe ni thina wa kutongesya nadu mate na kindu nakwa ndina kindu

**Translator :** Anasema ana shida mingi, yaani anasema alianza hiyo kikundi kama alikuwa na neno na sasa hana ni mzee na amekuwa vile unamuona sababu ya shida na anataka waangaliwe.

**Agnes Kisoo:** na vau nduivikaa vau

**Translator:** Amekomea hapo

**Com. Dr. Maranga :** Asante mama. Ngoja kidogo mama kuna swali unaulizwa.

**Com. Mutakha Kangu :** Mama umesema umeimba mpaka meno imepotea yote?

**Agnes Kisoo:** ii nambie ni mwiitu

**Translator :** anasema alianza kama alikuwa msichana

**Agnes Kisoo:** na nai na maeo on the nayu ndina mo

**Translator :** Na alikuwa na meno yote na sasa hana.

**Com. Mutakha Kangu :** Na kwa wakati huu wote hizi nyimbo kuna zozote mumeweka kwa cassette munaweza uza?

**Translator to Agnes :** ivinda yiu yoonthe ve mbathi mwekie vandu ta kasetini mwithie ni mutonya uta?

**Agnes Kisoo:** twonaa mundu wa utwita nisyosawa na tuyonaa mundu wa ututungia akatwikia vandu

**Translator :** Anasema wakati wanaimba zinajukuliwa kama na media na wahaoni response.

**Com. Mutakha Kangu :** Hawaoni?

**Translator:** Hawaoni.

**Com. Mutakha Kangu :** So maombi yenu ni kwamba kama kuna watu wakuimba kama nyinyi wapate njia ya kusaidiwa, kama wanaitwa kuimba wawe wanaimba kwa kulipwa hapana kutumiwa bure? Si ndio hivyo?

**Translator to Agnes :** kwou thina wenyu ila mweetwa mukaine withie nimutonya kuivya ni mwithia muyina mana

**Translator to Commissioner :** Anasema hivyo



**Com. Mutakha Kangu :** Asante.

**Com. Dr. Maranga :** Okay asante mama, nashukuru. Tuweke sahihi kitabu chetu rasmi. Mwingine anaitwa Musyoka Nthenge, Musyoka hayuko, Gideon Kilungu? Haya karibu wakati ni wako.

**Gideon Kilungu :** Nitawa Gideon Kilungu

**Translator :** Anaitwa Gideon Kilungu

**Gideon Kilungu:** na ni musili wa utui

**Translator :** He is a headman of a village. He is a headman of Mathumbili village Mwala.

**Gideon Kilungu :** na thina ula munene ningulasya silikali kana niteethiwe na thina munenen Kenya wa asili on the Kenya. Nundu mayonaa utethyo na me silikalini, na yila maundu mooka wiwaa twaiya musili. Na ti kundu musaada ona umwe twonaa.

**Translator :** Anasema shida kubwa iko na headmen sasa wao wanafanya kazi mingi kitu ikikuja ni wao wanaulizwa kutangaza na hawapati chochote kutoka kwa serikali.

**Gideon Kilungu:** kwou twikulasya Katiba tene no twi ma Kenya na nundu undu wonthe uthukumi munene withiwa na asili ma ndua

**Translator :** Anauliza Wa-Commission kama wao ni wana Kenya sababu ndio wanafanya kazi yote na hawapati chochote.

**Gideon Kilungu:** vau nivo ngwendaa ukulya twaie va nthini wa silikali Kenya asili ma ndua?

**Translator :** Anauliza mahali headmen wamepotelea katika Constitution.

**Gideon Kilungu:** Nundu ona tuinengawe kindu tuyikaa ata, ile kutangaswa, ila kwi otumuvothi twa DO o sub-chief o chif twiawa ika uu, ika uu, ika uu, tene mundu wiana takwa aile uthukuma mana ata?

**Translator :** Wakati kitu kinakuja watangaze ndio wanatangaza kama ni kukusanya pesa kutoka kwa wananchi ndio wanatumwa kukusanya na hawapati chochote na anauliza mzee mzima kama yeye anaweza fanya kazi bure mpaka lini?

**Gideon Kilungu:** Niviva vau.

**Com. Dr. Maranga :** Asante mzee (inaudible) kikao chetu rasmi na umengoea . Haya yule anayefwata. Dickson Mwanja.  
Dickson Mwanja?

**Dickson Mwanja :** Mtaniruhusu ni simame kwa sababu huwa nasimama kama naongea

**Com. Dr. Maranga :** Ni sawa.

**Dickson Mwanja :** Kwa majina ni Dickson Mwanja Mutisya kutoka (inaudible). Kikundi changu kinaitwa Health Care Promoters. Mimi kile ambacho nitaongea ili ikiwezekanavyo Katiba yetu itayoundwa sasa iwe ni katiba watu wote, vyama vyote kwa sababu wakati huu tunao sasa kuna vyama vingi lakini hakuna kazi watu wengine wa vyama vingine wakitaka kukuwa na mkutano hawaruhusiwi. Wakijaribu kufanya mkutano watu wa KANU wanatumwa na AP na mapolisi washuta wale watu wanaumiza bure, kwa hivyo katiba yetu iwezekanavyo iwe ni ya watu wamepata uhuru kamili tuwe tuna uhuru wa vyama vyote.

Na kitu cha pili serikali tuliyo nayo sasa, haitoi huduma kwa pande zote. Kama ni upande wa upinzani, hawatoi huduma kwa hivyo tungetaka katiba tunayotaka kuunda sasa, iwe kama ni upande wa kama Mwala ni upande wa wapinzani huduma ikitolewa itolewa pande zote ili iwache kutolewa upande moja kwa sababu upande wa upinzani hatupewi huduma.

Kingine ambacho ningetaka ni mkijaribu kufanya katiba yetu iwe nzuri ni kama Rais wetu sasa tunaye sasa amepewa madaraka makubwa ambayo imepita kiasi. Hata akitaka kufanya nini, akitaka kusema nichukuliwe saa hii nifungwe milele anaweza kusema ili awe ni Rais ambaye anaweza kuonywa kama amekosea awe mtu wa kuonywa si mtu above the law. Tuwe na Rais ambao si above the law.

Kitu kingine ambacho nataka kuingiza kwa katiba wakati huu sasa serikali ya Local Government imechukuwa wale watu ambao ni maskini waendee kuwa masikini kwa sababu kama County Council, wale wamama wanaouza vitu huku masokoni hata kama anachukuwa kitu ya shilingi kumi mpaka lazima atoe pesa, sasa wamama hawapati uhuru wa kuuza vitu vyao. Kama mtu anashona na charahani mahali nje anakuja anaambiwa utalipa kodi ya shilingi elfu sita license. Sisi ni kama hatuna uhuru kwa sababu wale watu wa Local Government wangeangalia huyu hana nini hana chochote hana soko. Wangejaribu kumwambia toa shilingi kumi kila siku kwa sababu huna mahali pa kupata kitu. Kwa hivyo ile katiba tunaounda sasa tunataka iwe ni katiba ya watu wanaoangalia watu wa chini, wale maskini ili ndio wainuke wafikie wale wengine.

Nataka ni malize tu kwa sababu sikuwa na mengi. Kitu kingine, katiba tuliyo nayo sasa imewapa madaktari uhuru kupita kiasi. Watu wengi wanakufa mahospitali daktari akifika hakuwa anaandika kwa kitabu nimeingia, yeye anatoka anaenda kwa clinic yake wale watu wako hapo hospitali wanakufa, hawana dawa, dawa zote wamechukuwa wamepeleka ma-clinic zao. Kwa

hivyo, serikali ingefaa tuwe na katiba inaohusu daktari na kazi moja kama amejiriwa ajiriwe, lakini si mtu wakufanya kazi mia moja na yeye ni mtu mmoja.

Kwa hivyo nitakachomalizie nacho ni upande wa Police sasa tumeangaika sana ukitaka kwenda Machakos ni shida kwa sababu mapolisi wote wamejazwa kwa magari wakifika pale wanapewa off, wale watu wanatoka pale wanaanguka na lile gari kwa sababu watu wanajazwa kwa gari kama nini. Na hii ni kitu kinaonekana wazi kila siku lakini serikali haichukui hatua. Kwa hivyo tungefaa tuwe na katiba inaoruhusu polisi akipatikana na, mtu akipatikana amebaba watu saidi kupita kiasi ashtakiwe na yule polisi akipatikana amehongwa afutwe kazi. Kwa sababu anataka kuua watu. Hivyo kwa sababu ninona wakati ni mfupi upande wangu nitamalizia hapo.

**Com. Dr. Maranga :** Bwana Mwanja kuna swali moja.

**Com. Mutakha Kangu:** Bwana Mwanja wewe unaona ni utaratibu gani tutaweka kwa katiba wenye utahakikisha serikali haifanyi mapendeleo ya kukataa kupeana huduma kwa sehemu za upinzani?

**Dickson Mwanja :** Unajua hapo siwezi kukwambia tutafanya nini kwa sababu hata tukisema tu – tungeomba tu katiba inayoundwa sasa iwe inapendelea sehemu zote kama ni upande wa upinzani wapewe huduma sawa sawa, kama ni yule Mbunge wetu tunaye hapa Mwala apewe uhuru wa kutunza watu wake kila wakati wakikutana nao. Ili wapeana mashida yao na kama wana shida pia wapeane. Wakati huu hatuna uhuru wa kuuliza Mbunge wetu. Mbunge akitaka kukutana na sisi hana nafasi.

**Com. Dr. Maranga:** Asante Bwana Dickson Mwanja. Yule anayefwata ni Anne ----- Una dakika tano mama. Unaongea kikamba?

**Anne Wausi:** Nitawa Anne Wausi

**Translator :** Anasema anaitwa Anne Wausi

**Anne Wausi :** yu nikulasya ii?

**Translator :** Anauliza hivi

**Anne Wausi :** nai ona machief na nimaiviwe

**Translator :** Walikuwa na Chief na wamelipwa

**Anne Wausi :** ala twambie namo

**Translator :** Walio anza kazi na wao

**Anne Wausi:** na ithye tiendea o mana

**Translator:** Na wao wanafanya bure.

**Anne Wausi:** yu muitumanthie o ka wikwa nundu tukee uumwa

**Translator:** Watafutiwe njia ya kuwasaidia kwa sababu wanatukanwa.

**Anne Wausi:** syana syitukulya tiendaa naku?

**Translator:** Watoto wanauliza, hii ni kazi gani mnafanya?

**Anne Wausi:** ute kindu

**Translator:** Haina chochote.

**Anne Wausi:** mutate utumathia kana nimutwonea o kaundu tikwa

**Translator:** Watafutiwe kama wanaweza pata chochote.

**Anne Wausi:** Nundu nitwanoie muno

**Translator:** Kwa sababu wamefanya kazi sana na wamechoka sana.

**Anne Wausi:** miaka mingi teumanya umitala

**Translator:** Miaka mingi hawezi akaahesabu.

**Anne Wausi:** utuendee

**Translator:** Wakiendelea na kazi.

**Anne Wausi:** ite kindu

**Translator:** Ambayo haina chochote.

**Anne Wausi:** nyie ndiumukulasya ii kana nimwona okawololo vandu?

**Translator:** Anauliza kama msaada wowote unaweza kupatikana kutoka mahali popote.

**Anne Wausi:** ndina mbingi, tumanthie wikwa

**Translator:** Amekomea hapo.

**Com. Kangu:** Asante Anne Wausi. Ninayemwita sasa ni Peter Katumbo. Dakika tano.

Anza na majina yako kamili.

**Peter Katumbo:** Commissioners of the Constitution, ladies and gentlemen. My name is Peter Katumbo. I happen to be the chairman of Makutano Palms Growers Association and also I am the Provincial Representative from Eastern Province and the so called Kenya Horticultural Crops Development Authority no, Kenya Horticultural Farmers Association. Well, mine is based on horticulture.

It is written and I will read, I will go through. First, is on subsidy to horticultural farmers. As the horticultural sector has become very important in the economy of this country in earning the foreign exchange, I take this opportunity to request the Commission, to give subsidy to farmers in order to caution them against escalating prices on agricultural inputs such as fertilizers, chemicals and machinery. For example, enough suckers palms to (inaudible) the very very (inaudible).

The small-scale farmers are harvesting hardest hit and if such subsidy is availed to them, the sector can improve greatly. These farmers can improve their standards of living and manage to educate their children and possibly minimize numerous harambee fundraisings prevailing all over the country.

Fuel prices: I also feel that the fuel should be subsidized so as to make it possible for the horticultural crops to be air freighted or shipped to Middle East, Russian Gulf or European union. This will again caution the agricultural farmer and the exporter of such commodities against the prohibitive high transport costs prevailing and make reasonable profits to their lives. I understand some countries have been doing this sort of thing for many years, for example S. Africa. That is all.

**Com. Kangu:** Thank you. A question?

**Com. Maranga:** You have mentioned the question of subsidies and instances that will improve lives, do you have any view to give about the liberalization process that is taking place in our country to vis-a-vis your cry for subsidies and prices. What appears to be price controlled?

**Peter Katumbo:** Thank you. Well, I think that is a rather shaky question and actually needs the...special studies in that when we talk about liberalization of the economy, may be goods but it hurts in some areas. For example, a very small...let me mention one thing. For example, let's talk of horticultural farms, e.g. let's take oranges or tangerine which come from Tanzania. Well you find the Tanzanias have found Nairobi our city, let's say they have ...rather they are in paradise, in that they take their oranges from Tanzania ... now, we are on liberalization, I mean tangerine, oranges from Tanzania, they will bring them to Nairobi, one bag is in the region of Ksh. 800.

To them, as you are aware that one Kenya shilling is equal to ten Tanzania shillings so, you find that one bag here in Kenya is Ksh. 800, to them it is Ksh. 8,000. So they find that, well in Kenya things are so nice, we are getting good money, they come here, they sell actually. But, unfortunately Kenya will never sell a single orange or tangerine in Dar es Salam or Arusha. Their shilling if you look at it I can say that it's value iko chini. Kwa hivyo the Kenyan farmer has been hit or rather anaumia. Kwa hivyo maneno ya liberalization because they are bringing their produce, they are selling these goods to get good money. Whereas when they bring their cheap oranges here and tangerine, the Kenyans aren't getting anything by selling their fruits in Nairobi because the market is flooded by cheap Tanzanian fruits.

**Com. Maranga:** It is your view therefore that we should protect our farmers, we reject liberalization or we take liberalization in certain measures.

**Peter Katumbo:** Certain measures, you are right.

**Com. Maranga:** Thank you.

**Peter Katumbo:** There must be a protectionism policy to a certain extent. Thank you, asante sana.

**Com. Maranga:** Sign in our official book. Now we have, the next one is Mukunya Nzioka? Mukunya Nzioka?

**Mukunya Nzioka:** Isyitwa yakwa nitawa Mukunya Nzioki

**Translator:** Anaitwa Mukunya Nzioka.

**Mukunya Nzioka:** ya keli, group ino yaitu Chairlady amin auneena tuineenaa, tuatiaa chairlady.

**Translator:** The second thing, the chairlady of the group akimaliza kusema wao hawaongei.

**Mukunya Nzioka:** aie

**Translator:** She has nothing to say.

**Com. Maranga:** Okey, wacha niwaelezee namna hii. Kama umeandika jina hapa na hutaki kuzungumza hata nikikuita, ni vizuri useme hutaki. Sawa sawa? Mwingine ambaye namuita ni Sowia Kioko. Anataka kuongea? Okey. Ama maoni ni ile ile?

**Speaker from the audience:** Wameshaandika. Ni ukweli?

Kwa hivyo hakuna....Okey. Thank you very much. From here, I have MacDonald David Muli. MacDonald. Hayuko? Juliana, huyu ambaye ana-register nataka kuongea na wewe. Wakati una-register watu ujue wale watu ambao wanataka kuongea. Watu wanaweza ku-register lakini hawataki kuongea. Kwa hivyo wana haki hiyo. Kwa sababu sasa majina yakija hapa mimi nafikiri kila mtu anaongea na wengine hawataki kuongea. Yule anayefuata ni Gideon Nzioki, si aliongea? Huyu ni mwingine. Haya ingia.

**Gideon Nzioki:** Not right now. Right now I am not going to talk. (inaudible)

**Com. Maranga:** So you have already prepared?

**Gideon Nzioki:** Yes, I have prepared the memorandum. Not right now, I will hand it over when you come to the views, when it is finished. So, thank you very much. I have not registered. Thank you.

**Com. Maranga:** Next is Juliana Muli. Juliana Muli? Huyu kama hataki kuongea sawa. Unataka kuongea? Muulize kwanza hapo. It is her constitutional right. Aanze.

**Juliana Muli:** Isitwa yakwa ni Lucia Nzule Muli

**Translator:** She is Lucia Nzule Muli.

**Com. Maranga:** Lucia ama Juliana?

**Translator:** yu thina ula niwawo ii ni kwithiwa wathini uu, nayu wathi uu ndina ndikindu ngunewa

**Translator:** Shida yake ni kuitwa waimbe na hapati chochote.

**Juliana Muli:** na indi ninakuie vo, ona ii myaka yu ndimisi nundu nimukuu

**Translator:** Ameimba kwa miaka mingi, hata sasa hawezi akahesabu.

**Juliana Muli:** na ninaa mana na ningwenda nimathiwe kaindu, nikiw'e nivuiwe kaw'u withie nineewa muyo na ndisiwa na ngali ngaine nde maeo ona yimwe. Ate yimwe ikyamanu

**Translator:** Anasema anataka aangaliwe, atafutiwe kitu.. Kama ni kuimba aimbe akiwa na furaha.

**Juliana Muli:** Ngaikaa ukulya ni syana mwaitu watuetee ki? Nakw a ndi kindu ninaete na nininoie ituo nikusunga

**Translator:** Ndio aache kuulizwa na watoto, mama umeleta nini? Na yeye hakuleta chochote. Na vile anachoka na kuimba.

**Juliana Muli:** na nienda yu ndisiwa nisiwe vaa na ngali, ndikinya na kuu na ndinewa kindu, nienda niwae muyo.

**Translator:** Anasema anataka kama anaitwa mahali, gari ipelekwe wachukuliwe huko na wakimaliza kuimba wapatiwe kitu, wapelekewe watoto nyumbani. Na yeye anakomea hapo.

**Com. Maranga:** Asante mama Lucia Muli, utatuwekea sahihi kitabu chetu. Sasa mimi naona wengine ambao wako hapa ni ile group, sijui kama wanataka kuongea. Wacha niwaite kwanza. Halafu enda hapo uwaulize kama, if they want to speak, if they don't it is not necessary. Tabitha Matheka. Unataka kuongea? Ngile Muli? Ndio huyo? Rhoda Kaembe? Anataka kuongea? Mwingine anaitwa Kamene Nduti? Anataka kuongea? Haya ingia.

**Kamene Nduti:** Nyie thina wakwa no ula wanenganwa ni chairlady wa kwina

**Kamene Nduti:** Nitawa Kamene Nduti

**Translator:** Anaitwa Kamene Nduti

**Translator:** Shida yake ni ile imeongewa na Chairlady wa kuimba. Hakuna kingine.

**Com. Maranga:** Okey. Next anaitwa Kaloni Kituku. Anataka kuongea? Ama ni yule Chairlady amezungumzia? Okey. Anne Mutuku. Anataka kuongea ama ni vile chairlady ameongea? Okey. Thank you very much. Give me the next list. Kavee Michael? Okey. Sawa. You want to talk in English or Kiswahili?

**Rosalyn Kavee Michael:** In English. My names are Rosalyn Kavee Michael. Many pupils said that they need free education, free basic needs, free medical care when a patient is admitted. No divorcing.

**Com. Maranga:** Divorcing?

**Rosalyn Kavee Michael:** Divorcing. No taking of drugs. No polygamy. Land should not be sold without children's notice.



**Com. Maranga:** Okey. Just a minute. Any question?

**Com. Ayonga:** You have said no divorce?

**Rosalyn Kavee Michael:** Yes.

**Com. Ayonga:** Now, when two people disagree, what would be the solution? The lady doesn't want this man. He has been beating her too much and she wants a divorce or the woman is not good to her husband. What would you like to be done? You can't just say no divorce.

**Rosalyn Kavee Michael:** The Government to care for the children.

**Com. Ayonga:** And allow the divorce?

**Rosalyn Kavee Michael:** No.

**Com. Ayonga:** Thank you.

**Com. Maranga:** Okey. Thank you very much. Please sign and give us that memorandum, we need that. Then we have Redempta Mutuku.

**Redempta Mutuku:** Kwa Chairman and the Commission, ladies and gentlemen. Asante sana kwa wakati huu. Ningeongea kidogo juu ya ile inawahusu disabled, the sick and the poor. Mimi naitwa Redempta Mutuku. Huko katika villages kule tumetoka kuna walemavu, wale watoto wamezaliwa viwete, wamezaliwa hawajiwezi, wengine wamekuwa wagonjwa. Kwa mfano hata kama mtu amezaliwa kiwete au amezaliwa namna gani, yeye ni wa Kenya na ni unaona ni kama hawajulikani na ni kama hawasaidiwi.

Kwa hivyo mtu anafanyika hivi anakuja kukufa na shida bila kujulikana. Na kuna wale wamepata magonjwa yale magumu ambayo hayawezi kutibiwa na dawa hizi rahisi rahisi na ni kama hakuna mahospitali kwa sababu pale unapeleka mtu unaambiwa huko na wanaitwa cost-sharing. Hii cost-sharing, ni kitu tu unaandikiwa. Unakuja na kitabu chako unaandikiwa, unaambiwa nenda ukanunue dawa. Kwa hivyo, cost-sharing inatushinda kuelewa ni ya nini na ile dawa inaweza kwenda ukauziwa pesa nyingi huwezi kupata, kwa hivyo yule mtu anakufa tu. Kuuliza kwangu ni hivi, kungewezekanaje hiyo mambo ya cost-sharing iondolewe kwa sababu inatumiza sisi? Hiyo ni moja.

Pia ningependa kuongea juu ya umaskini. Kuwa maskini sio kupenda kwa mtu na wengine wamekuwa maskini, wanakuwa hata wamezaa watoto, hata wanakufa na magonjwa ile ya shida kama Kwashiokor na Marasmus na vitu kama hivyo. Ni kwa sababu hawana kitu cha kuwapatia hao watoto na hawajiwezi. Hakuna mtu anachukua mtoto wake lakini inakuwa hana nguvu ya kulinda yule mtoto. Ningeuliza kama ikiwezekana watu kama hawa wanaweza, kama tunaweza kufikiwa, sisi hatupitiwi, tuko mbali sana. Tuko mbali sana.

Kutoka kule juu tuko mbali sana. Na kwa hivyo kama kunaweza kuwa ana kitu tukawakarimu kidogo ili tukawa tunaweza kufikiwa. Pia ningependa kuongea kidogo juu ya kitu niliona wanaita land transfer. Hiyo inakuwa ni shida sana kwa.....umelipa pesa nyingi, ulipe wale watu wanasema ni wa survey. Na tunaambiwa mpaka land ni yako ama ni ya babako, au ni ya bwanako na inachukua hata mwaka mzima, miaka mitatu mpaka hata wewe unakufa unawacha ile land si yako, hujui ni ya nani na shida inaanzia kutoka hapo. Yaweza kuwa watoto wale ulizaa hawana uwezo kwa hivyo, nao watanyang'anywa na mtu tu na wizi ni mwingi huku Kenya. Kuna kitu kama kusema ati unampatia heshima kitu cha mtu. Kwa hivyo kuuliza kwangu ni, kama ile procedure ya ku-transfer ile land kutoka kwa mtu ingekuwa free. We pay a lot of money. Kama ingekuwa free. Kwa sababu kama hao ni wafanyikazi wa Serikali, si Serikali...sijui nini hapo.

Pia, ningependa kuongea juu ya salaries kidogo. Mimi si mfanyikazi, I have already retired lakini ningependa kuongea juu ya mambo ya mishahara. Kama vile watu wa hapa chini wanaumia sana, wanafanya kazi mingi sana. I take an example of teachers, vile wanafanya kazi, wanafanya kazi hata usiku. Hata 24 hours. Hakuna hata kupumzika na ile kitu wanalipwa ni kitu kidogo sana na tukisikia kule juu, kule juu kabisa, wacha mimi nitaje Parliament kwa sababu si jina la mtu. Ningependa kama inawezekana kitu kama comparison ifanywe kidogo. Kwa sababu ile tofauti iko ni kubwa sana na ile kazi inafanywa na mtu mdogo ni nyingi sana na analipwa kitu kidogo sana. Wakilalamika wanaambiwa kama ni striking, you are going home. That is unfair.

Ningeuliza kama mambo kama haya. Pia ningeuliza, inawezekanaje? Mtu hawezi kujifanyia mishahara wake. Itakuwa vibaya sana kwa mtu kuandikwa na hajui...sijui aandikwe au ajiandike na aseme mimi nitakuwa najalipa kiwango fulani. Kwa sababu uki-compare na ile kitu hawa watu wa Parliament wanalipwa na other firms haziko sawasawa. Ile wanalipwa wenyewe au wanajilipa wacha niseme hivyo. Ile wanajilipa ni nyingi sana hazistahili. Hata mimi nimefanya kazi maisha yangu yote na nikaenda retire na ile nimepewa, I could not be equivalent to mishahara wa mtu mmoja kule Parliament.

Kwa hivyo inawezekanaje, wakafikiwa ni kwamba, hii kwetu inatumiza. Hawezi kuchukua kile kitu chote kiko na sisi hapa chini tunaumia. Sijui kama muda wangu umekwisha?

**Com. Maranga:** (inaudible) umemaliza? Thank you very much. Tuwekee sahihi kitabu chetu rasmi. Thank you very much. Yule mwingine ambaye naita sasa anaitwa Ndambuki Nzuki. Very good, young man. Unaongea kwa lugha gani?

**Andrew Ndambuki:** English.

**Com. Maranga:** Okey. What you do, you start with your full names before you start giving us your views.

**Andrew Ndambuki:** My full names are Andrew Ndambuki Nzuki. The points which were given by Kianyoni pupils were; orphans must be cared for with high protection and basic needs. No dropping out of schools, causing unwanted pregnancies. Those who commit adultery will be jailed. Medical care should be free. The aged people should be cared for. Thank you.

**Com. Maranga:** Thank you. Excuse me young man, come and register with us and give us your memorandum. Bwana Program officer umechukua muda sana, unaona mwingine anaondoka. You wait, after her you register, you sign and then you give us that memorandum. Thank you very much. The next one is Eustus Nzioka? Not there? Mwendu Mwasi? Okey. You want to speak in English?

**Mwendu Mwasi:** Yes.

**Com. Maranga:** Okey. Then you start with your full names.

**Mwendu Mwasi:** My names are Maureen Mwendu Mwasi. Education has been quite expensive thus many parents are unable to send their children to school. Instead, very young girls become maids, house girls, and boys become houseboys and even street children. It does not guarantee us with jobs. The Constitution of Kenya should make education free and compulsory for all.

The Government should formulate a law protecting children against child labour and punish those practicing it severely. Job opportunities must be created and the education goals should be formulated to reflect the needs of present and future Kenyan child. The Government should make Constitution covering birth controls to allow parents to give birth to children they can educate and care for. That includes; the number of children per couple. Street children will be reduced.

Land: Children have a right to inherit land but most times parents sell land without caring what will be our fate. This makes us poor and even become displaced. The Constitution should make selling of land illegal. Children must be allocated land first and if there is surplus then it can be sold. The Constitution must protect children and allow equal rights on land inheritance. That is to both boys and girls.

The girl-child: Girls have been raped by their own fathers and others abuse them. This is in the increase due to killer disease H.I.V. Aids. Young girls have not been given equal rights than boys. In many communities in Kenya, they are given out for early marriages as early as ten years. Others leave schools for female genital mutilation leading to many deaths. The Constitution of Kenya must protect the girl-child by giving the penalty of rapists which has been very lenient to a death sentence to curb this

torture. The Constitution of Kenya should empower the Sub-chiefs to oversee customary marriages and to look at those practicing female genital mutilation and early marriages with serious punishments.

Freedom of worship: This freedom has made majority of Kenyans to involve themselves into funny cults which go to an extent of offering human life as sacrifices and more so children or the school girls. As young generation, children are threatened by funny people killing them and scooping their private parts, breasts and tongues. This resulted to many deaths and yet none has been presented for this. The Constitution should protect children from such practices and give limits to the freedom of worshipping. Such people practices involving children as agents should be given penalties closer to death sentence.

Civic and parliamentary terms: Some MP's and Councillors have become a threat to the County Council and Parliament. Some have been there since independence, when they lose seats, they get nominated. As children, we are also growing and eyeing the same seats. The parliamentary motions bore them and end up sleeping during debates or absent themselves. We recommend two terms. i.e One should serve as an MP or Councillor for two terms and retire to give chances to the others. All the best and success as you accomplish the tough task. Thank you.

**Com. Maranga:** Thank you very much. Those are very good views. Let me know whether any Commissioner wants to ask a question. No, please register with us and give us your memorandum. Alright. Thank you very much. Very bright young girl. Thank you. The next one is William Mwathe Kimongo. Kuja upande huu na uanze na majina yako. Sijui utaongea lugha gani?

**Kimongo Mwathe:** Mimi ni William Kimongo Mwathe ama Mwathe William Kimongo. Mimi nitaongea kwa Kiswahili na sijui sasa kama nitaanza.

**Com. Maranga:** Anza.

**Kimongo Mwathe:** Okey. Mimi nitaongea juu ya mipaka. Wakati ambao tulipatiwa uhuru, mipaka iliwekwa katika kila Province. Nyuma yake, sehemu zingine za district nyingine zikaanza kubadilishwa na mipaka ilikuwa inawekwa ya kawaida wakati Sir. Berlin ali-declare emergency, Sir Patrick Hedson na nyuma yake MacDonald ambaye alitukabidhi uhuru wakati huo. Mzee akachukua na ningetaka kusema, kuonyesha mahali moja ambao mipaka ilibadilishwa. Kama ukienda Athi River utaona Portland Cement na mpaka uko hapo mbele wa Machakos district na unaenda mpaka huko mbele na sehemu hiyo ilikuwa mashule ambayo ilikuwa huko ilikuwa inaendeshwa na County Council ya Masaku. Nyuma yake sasa ukienda huko hata udongo imekuwa kama ni ya Kajiado.

Hiyo ndio imenileta kusema kwa committee hii, hiyo mipaka iweze kuhifadhiwa. Kwa sababu vile mnasoma India na kwingine, mnaona mipaka imeleta taabu sana na vile vile katika district ya Machakos mnakumbuka Kilimambogo Teachers College ilikuwa katika Machakos district. Mipaka ambayo imekuwa declared wakati huo na mkoloni kabla hajaenda ilikuwa pande hii

ya Machakos mpaka karibu Thika.

Ukivuka huko ukipata njia ya kwenda Tana river, utaona mpaka inaenda mpaka Tana river district ya Machakos na inapita mpaka Chambele karibu tunapakana na Kitui. Hiyo ingine ni sawa. Mahali pengine kutoka hapa kwenda kama Thika kwenye mananasi, sehemu nyingine huko ingali ya Machakos district na hiyo italeti taabu nyuma yake. Hiyo ya mipaka nitakoma hapo.

Ningetaka sasa kuongea habari ya uchawi: Katika wakati mwingine niliona taabu katika High Court Machakos. Kulikuwa na Mhindi mmoja alikuwa Judge katika Court na kulikuwa na mama mmoja wa Mutomo ambaye alikuwa ameuu mama yake na huyo mama kesi yake ikaendeshwa na ikawa vile aliuu mama yake, ni lazima apewe adhabu ya kifo. Wakati huo niliona Assessor, waliulizwa kama kuna uchawi na walimwambia yule Judge Wakamba pande hiyo, wangali na uchawi. Huyo mama akahukumiwa kifungo cha miaka nne na vile vile Judge alikuwa anauliza kama kuna kitu ya kabila hiyo ambayo huwa katika sehemu hii ya Ukambani.

Ningetaka hiyo sheria iwe inaangaliwa kwa sababu niliona inatatiza Ma-Assessor wakati waliulizwa hiyo. Tena, ile ingine ningengea juu ya korti. Tuseme korti yoyote. Watu siku hizi wamekuja...tulifanyiwa Land Adjudication mashamba yetu na ikawa na mipaka. Mtu anang'oa mpaka, mpaka anaenda kwa shamba ingine na korti ikifanya kesi, ukienda kortini inarudi, inarudi, mpaka nenda rudi haina mwisho. Nilikuwa nikisema ni maoni yangu kuwe na sheria ya korti. Ipatiwe uwezo, kukiwa na kesi kama hiyo ya mipaka na vitu, kwa sababu mtu anaharibu mpaka anang'oa miti na kila kitu, sasa akienda kortini anakataa.

Ningetaka Commission ihakikishe kesi ya namna hiyo, korti inapatiwa mandate ama inapatiwa ruhusa kwenda kutoa korti ihame katika korti mpaka kuenda kuona. Kwa sababu makesi imerundi kanwa mpaka kortini mpaka juu na juu. Iwe inahamishwa mpaka kwenda kwenye hiyo kesi na mtu analipa gharama. Let us pay the transport na mafuta na kila kitu halafu Judge anakwenda huko na mashahidi wanakaa kwa shamba hiyo ndio imesumbua watu. Halafu kesi ziwe zinaamriwa kwa haraka. Hiyo ndio nilikuwa ninataka kuongea.

Ile ingine na labda imeletwa ama haijaletwa. Tumekuwa na taabu, mtu anaoa bibi, bibi anahama, anaenda pahali ingine anakaa mwaka nenda rudi, anarudi. Mzee ameo bibi mwingine na wako watoto na ametafuta mali na bibi yule ambaye yuko. Halafu bibi yule akirudi, yule akirudi, bibi ama watoto, wanakuja kusema wana kifungu cha mali katika sehemu hiyo na bibi mwenyewe yule aliolewa, alizaa watoto, wakatafuta mali, akakuta kulikuwa hii, kulikuwa na mashamba ambayo hayakuwako na imetafutwa na mama huyu. Huyo mama kama bwanake amekufa ama awe, inakuwa na taabu. Sheria ya kabila hiyo inataka irekebishwe iwe ni sawa. Mambo ambayo ilikuwa imenileta nafikiri ni hayo.

**Com. Maranga:** Thank you very much Mzee William Mwathe. Kaa kidogo kuna swali utaulizwa na Commissioners.

**Com. Ayonga:** Mzee Kimongo, sikuelewa vizuri uliposema juu ya uchawi. Je kuna uchawi?

**Kimongo Mwathe:** Kuna uchawi. Uchawi unaweza kulinganishwa. Sasa kuna madawa ambayo mtu anaweza kwenda kuwekea mtu. Nimeona tokezi kama kuku zimewekewa shamba yako imekuwa kubwa, ambayo mnapakana shamba. Mtu anaweka dawa, ni kama hiyo tu, anaweka dawa. Uchawi kuna watu ambao saa ingine wanakutwa usiku wakifanya round katika mji wako. Sijui ni kitu gani anaweka, ni *kithangona*, kinaitwa *kithangona* ama kinaitwa kitu gani? *Kithangona*. Anaweka katika shamba hilo ili muwe mnapata madhara ya watu kupata accidents ama mambo mengine ya kutopata mali. Hiyo ndiyo inaitwa uchawi na hii inajulikana hapo mbeleni watu wa kabila hiyo wangali bado kufa wote. Wangali wako nazo.

**Com. Ayonga:** Ungelipenda tufanye nini katika Constitution?

**Kimongo Mwathe:** Tungetaka ikiwezekana mambo kama hayo, sababu hata inasumbua katika vile niliona katika korti, Assessor akisumbuliwa na kuulizwa maneno hayo, ningetaka irekebishwe, kuwe kuna mpango wa sheria. Sababu mambo hayo lazima yawe katika korti. Lazima ipatikane katika korti.

**Com. Maranga:** Mzee umezungumzia mambo ya mipaka ya mikoa na districts. Ukasema zamani Kilimambogo ilikuwanga Masaku, sasa iko wapi?

**Kimongo Mwathe:** Iko katika Chafuu na chini kidogo iko katika Machakos. Iko katika Murang'a. Iko katika Kiambu na ile ingine ilikatwa ikaenda katika Murang'a. Ukienda huko Ithanga karibu Mapoloni utakuta imegawa na ikawa na DO wa pande hiyo. Kama Ndithini, land market was Machakos County Council na hata ndio tulikuwa tunapeana plan na imekuwa transferred to Murang'a district. Hiyo ndio italeta vita nyuma yake. Mipaka ile iliwekwa wakati wa kicolony lazima ihifadhiwe. Kama Nairobi mahali inafika J.K. hapo mbele lazima ihifadhiwe na mpaka inaenda mpaka inapakana na areas zingine.

Hiyo ya Province ndio nilikuwa naongea. Ya district haina maneno. Kwa sababu vile tuligawa Makueni, tuli-agree wazee wa Machakos, district imekuwa na population mingi na ni lazima iwe katika district kugawa nyingine hiyo haina neno. Lakini ile mipaka iliwekwa wakati wa mkoloni, hiyo tunataka ihifadhiwe kwa sababu hiyo mambo haijakuwa changed na italeta taabu nyuma yake kwa miaka ambayo inakuja kwa watoto wetu waki-claim. Mahali ya mananasi Thika is part of the Machakos district. Watakuwa watoto wetu wanataka kwenda kulima huko na hiyo italeta fujo.

**Com. Maranga:** Asante Bwana. Thank you very much Mzee. Asante sana, Mzee William Kimongo. Tuwekee sahihi kitabu chetu rasmi. Asante kwa maoni yako. Nataka tu kukumbusha wananchi, hebu niwakumbusheni wananchi ya kuwa mkifika wale ambao wanataka kutoa maoni, ni vizuri mjiandikishe na vile vile nimeona wanafunzi wa shule wamefika. Pengine kama wangetaka kuongea mapema, tutawapa nafasi, kwa sababu tunajua wao ni wanafunzi. Kwa hivyo hiyo, I need to have that special recognition. Otherwise, yule ambaye namwita sasa anaitwa Teresia Wavinya Ndolo. Ndolo? Okey. Mzee wangu ongea pole pole kwa sababu huyu anaanza kuongea. Anza na majina yako kamili.

**Teresia Wavinya Ndolo:** Majina yangu naitwa Teresia Wavinya Ndolo. Mimi ni Mwalimu wa pre-school na kama Mwalimu wa pre-school tuko na shida sana juu ni sisi tunaanzisha msingi ya watoto kutoka nursery na wanaenda kwa Primary school mpaka wanaenda University na hatuna mshahara. Hatuna watu wa kutulipa.

Tukiuliza juu ya mishahara yetu, tunaambiwa tulipwe kama watchmen. Pesa zitolewe kwa shule halafu baadaye tulipwe. Tulipouliza kwa nini, tukawachiliwa hivyo tu. Tukaambiwa tuwe tunakusanya pesa halafu tunajilipa. Sasa ndio ninataka kuuliza, kwa nini hatuwezi kulipwa na Serikali? Kwa sababu hao wazazi tu ndio tunawasomeshea watoto na wengine wako na shida sana. Mtu anakuja tu analipa shilingi hamsini, mia, hatuwezi tukapata mshahara wa kutosha na tunaamka asubuhi, --- ikifika miaka yake akijisikia anaenda nyumbani tu na hakuna pension. Kwa hivyo tunauliza kama tunaweza kupata pension mtu akimaliza miaka ya kusomesha.

Ningependa kuuliza kama tunaweza kupata mishahara kutoka kwa Serikali, kama hiyo fees inaweza kuachiliwa juu wazazi wana shida sana.

**Com. Maranga:** Ni hayo tu? Asante. Register there na uandike jina lako na u-sign. Yule ambaye anafuata anaitwa Peter Kiilu? Hakuna. Dominic Mwau? It is your time now, five minutes.

**Dominic Mwau:** Kwa majina naitwa Dominic Mbatha Mwau.

**Com. Maranga:** Ongeza sauti ili wakusikie. Kama una memorandum, give us the main points.

**Dominic Mwau:** Nilikuwa na moja ya kikundi na nilikuwa na ingine yangu ya kuongea. Ningependa kuongea juu ya zile majina ambayo ni ya Kizungu na bado inaendelea katika hii district yetu ya Ukambani. Kwa mfano kama hii ingine ya Machakos, tukiangalia katika maandishi ya Kikamba hakuna 'S' inaishia. Tena hakuna 'C'. Kwa hivyo naona ningependa tubadilishe majina tutumie ile yetu ya kienyeji. Badala ya kuitwa *Machakos*, iitwe *Masaku*. Tena kama *Athi River*, hiyo ni jina ingeitwa *Mavoko*. Inginge ni kama *Kabaa*, *Kabaa* ukiangalia kunaye *B* na wakati wowote majina ya kikamba inaanzia, pahali iko *B* inaanzia na *M*. Sasa badala ya *B* wangeweka *V*. Ie ingine ningeeongea juu yake ni mambo ya usalama.

Tuseme kama hii uwanja ya Nairobi, watu wanasumbuliwa hapo sana wakionyeshwa mahali pa kwenda na mtu hawezi kutoka nyumbani akiwa hajui mahali anaenda. Saa ingine unaona mtu ananyang'anywa briefcase na polisi bado wanaangalia. Hiyo pia ningeeongea juu yake. Ikiwa kunaye usalama, mtu awe na uhuru wa kutembea, na asianze kuulizwa maswali, ati unaenda wapi? Unataka kuonyeshwa gari. Kwa sababu wezi wamechukua hiyo jukumu ya kuonyesha watu na ni njia ya kuiba.

Ile ingine ningeeongea juu yake ni mambo ya utawala. Mimi kwa upande wangu ningependelea kama ni mambo ya Ma-DC, Ma-PC, hata Ma-Chief na Ma-Assisstant Chiefs wawe wakichaguliwa lakini siio kuandikwa na ikiwezekana, mtu achaguliwe

sehemu yake yaani sehemu ambayo anatoka.

Kitu kingine ningeongea juu yake ni hizi ada ambazo watu huwa wanapewa na Serikali kama kitambulisho, passport na birth certificate. Huwa ziko na taabu sana kuzipata. Sasa sijui kama kunaye nini...itawekwa ya kurahisisha. Watu wawe wakiwa wanapata kwa njia ya rahisi. Kwa sababu kama passport, mtu anasumbuka mpaka kama alikuwa na haja ya kuenda mahali, anawacha. Inachukua muda kupata. Ni hayo tu. Mengine yako katika memorandum.

**Com. Maranga:** Asante kwa hiyo memorandum yako. Eka sahihi katika register rasmi. The next one is Julius Mutua Ngilu. Yuko? Next is Justus Mwoki Mativo. Mativo? The next one is Evanson Mwavulu. Evanson? Wacha tumsikize Evanson.

**Evanson Mwaluko:** Majina yangu ni Evanson Nzigo Mwaluko. Not Mwavulu? Mwaluko. Mimi ni mwenyekiti wa kikundi kinachoitwa 'Mumo self-help group' ambacho kiko katika Masii. Kiko na members mia moja na wale active ni sabini na tano. Hiki kikundi ni cha kusaidiana kama maneno ya school fees, kama mtoto mmoja amelemewa na fees, tunamchangia. Saa ingine tunakuwa na project ya kuweka kuku, mbuzi, na hivi sasa mwaka huu tunaazimia kuanza '(inaudible) project. Naomba radhi kwa vile nilikuwa nimetengeneza memorandum na kwa bahati mbaya hakukuwa na stima, kwa hivyo sikuwa nayo na pengine mkiwa ofisini nitawaletea. Ikiwa typed.

**Com. Maranga:** Kama umeandika na mkono ni sawa tu.

**Evanson Mwaluko:** Imefungiwa.

**Com. Maranga:** Okey. Present the main points.

**Evanson Mwaluko:** Ile tumeonelea ni maneno ya Parliament. Parliament tumeonelea, hatutaki iwe na uwezo wa kubadilisha Katiba. Maanake tumeona wakati mwingine Katiba inapelekwa Bungeni saa nane, saa nane na nusu inapitishwa na inakuwa sheria na sisi hatujaulizwa. Inakuwa imepitishwa na watu sabini na tano na sabini na mbili wamekataa. Kwa hivyo, hiyo ndio tunaonelea, tunasema Katiba iwe ya wananchi ndio wawe wakiulizwa vile wanataka, kama wanataka kubadilisha. Maanake hii vile tunaona Katiba ya Kenya imebadilishwa mara nyingi, mara nyingi, inaletwa saa nane na saa kumi inakuwa sheria yaani inabadilishwa.

Ile ingine ni maneno ya wananchi kuwa citizens: Kila mwananchi wa Kenya ako na uhuru kuwa citizen wa Kenya na ako na uhuru wa kuishi mahali popote atakapo Kenya hata kama ni biashara anaweka mahali atakapo Kenya. Lakini sio kama vile imekuwa, unasikia hapa, unaona, unasikia, pengine sasa kuna watu wako refugees in their own country. Kama vile ilitokea mwaka wa tisaini na mbili na tisaini na saba. Hiyo hatungetaka itokee na ni kukuwa na Katiba mbaya ile haiwezi kulinda sisi.



Ingingine ni maneno ya citizenship: Nimeonelea ya kuwa, mwananchi, kwa mfano mimi ninaenda ninaishi America, ninaoa America, nikileta bibi yangu atakubaliwa. Lakini kama ni dada yangu akienda kuolewa huko akileta bwanake, hatapewa citizenship. Hiyo ndio nataka iangaliwe sana maanake sisi wote tunasema ya kwamba Kenyans are equal.

Ingingine ni kuwa kila mwananchi wa Kenya anaweza kuruhusiwa kama ni kupiga kura, kwamba wakati huu tuko na shida ya kuchukua voters card kwa vile watu wengine hawajachukua. Wanatakiwa kitambulisho. Kwa hivyo anything ile inaweza kutambulisha mtu kama ni ID card, Passport, Birth Certificate ama Driving licence ama document yeyote ambayo inaonyesha huyo ni mwananchi wa Kenya, ako na uhuru wa kuchukua voters card.

Ile ingine ni ya kuwa, the President asiwe Commander-in-Chief of the Armed Forces. Commander-in-Chief of the Armed Forces, anatakiwa mtu amesomea hiyo kazi lakini sio mimi kama leo nimechaguliwa kama Rais, naenda kuwa Commander-in-Chief of the Armed Forces na sijui vile bunduki inashikwa, vile inasema. Sasa hiyo ndio naona saa ingine watu wetu wanatumiwa vibaya sana hata wanajeshi wetu wanatumiwa vibaya sana.

Ile ingine ni maneno ya boundaries. Hiyo ndio imesumbua wananchi sana Kenya. Maanake unaweza kuona pale ng'ambo ya barabara, district ikiandikwa hapo, inaweza kuwa hapa karibu na wewe. Pale ng'ambo ya barabara unasikia watu wanaenda district headquarter kama Makueni. Kwa hivyo hiyo tunataka iangaliwe sana. Hiyo imetusumbua sana, mtu anaweza kutoka hapa aende kwa DC na mguu na anaambiwa atoke hapa aende kama Makueni. Hiyo inasumbua sana maanake hii imekuwa ni kama, for example, mimi ni MP wa hapa na hao watu hawanisikii, nitasema hao wakatwe wapelekwe huko siwataki.

Kwa hivyo inakuanga kama ni political gift. District inapeana kama political gift. Ingingine ni kama constituency. Unaweza kuona mtu mmoja anawakilisha watu elfu tano na mwingine anawakilisha watu elfu mia moja. Kwa hivyo hiyo nataka iangaliwe sana, iwe ni kama, constituency ikatwe kama katikati ya watu, 45,000 na 70,000. Sio mtu awe anawakilisha kichaka ambacho hakina watu. Maanake sasa hii ya Kenya inaonekana inakatwa kama forest acreage na sio population. Hiyo inatakiwa iangaliwe sana.

Ingingine ni wananchi wa Kenya, tuko na shida sana. Moja, katika local authorities, sisi hatuna uwezo na hatuna say na sisi ndio tutawalipa hao wa Local Authorities. Ile kodi inakusanywa huko hatuna uwezo wa kujua imekusanywa ngapi kutoka kwa location yangu. Hii ndio inatakiwa na ingine Chairman kama tunataka vizuri, awe anachaguliwa na wananchi wenyewe. Lakini sio Ma-Councillors, sio eti Ma-Councillors wale wanaenda anawapatia pesa, unachukua, unakuta mtu ni thug na amechaguliwa Chairman. Huyo hakuna kitu atasaidia wananchi, kwa hivyo mtu awe kama ni chairman, awe answerable direct to wananchi. Lakini sio directly answerable to Councillors maanake unaona vile sasa, kama mimi ni Chairman na hawanitaki, leo wataungana, saa nane wamenitupa na hiyo ni pesa ya wananchi, taxpayers money inatumika.

